JUKWAA LA KATIBA TANZANIA

TANZANIA CONSTITUTION FORUM
P. O. Box 78466, Plot No. 201 Block 46 Kijitonyama, Adjacent to Kijitonyama UDSM Hostels,
Dar Es Salaam, TANZANIA
Tel: +255 22 2773795 Fax: +255 22 2773764 Cell: 0783 993088
E-mail: jukwaa.katiba@gmail.com,info@jukwaalakatibatz.com Web site: www.jukwaalakatibatz.com

MAAMUZI YA JUKATA BAADA YA KUKATALIWA KUFANYA MAANDAMANO YA AMANI YALIYOKUWA YAFANYIKE TAREHE 30 OKTOBA 2017

TAARIFA KWA UMMA

1. UTANGULIZI

Ndugu Wanahabari, tarehe 7 mwezi Oktoba 2017 JUKWAA LA KATIBA TANZANIA (JUKATA) tulitoa taarifa kwa umma kupitia vyombo vya habari kuelezea kusudio la kufanya maandamano ya amani nchi nzima siku ya tarehe 30 Oktoba 2017. Maandamano hayo yalilenga kuunga mkono jitihada za Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kusimamia rasilimali za taifa pamoja na kupiga vita rushwa. Pia, kufikisha ujumbe kuhusu haja ya serikali yake kurejesha mchakato wa katiba mpya ili taifa liweze kupata katiba mpya chini ya uongozi wake. Na kwa uzito huo, JUKATA lilimwandikia Mhe. Rais ili apokee maandamano ya kitaifa ambayo yalipangwa kufanyika kuanzia ofisi za JUKATA hadi viwanja vya Mnazi Mmoja. Hadi leo, JUKATA hatujapata majibu ya barua iliyotumwa Ikulu kwa Mhe. Rais juu ya ombi letu, ingawa tulipokea barua kutoka Jeshi la Polisi- Kanda Maalum ya Polisi, ikikataza kufanyika kwa maandamo ya amani ya JUKATA.

2. MAAMUZI YA JUKATA BAADA YA KUKATALIWA KUFANYA MAANDAMANO

Ndugu Wanahabari, baada ya JUKATA kupokea barua ya katazo la kufanya maandamano ya amani kutoka Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Polisi, tumefanya uchambuzi wa sababu zilizotolewa na kuridhika kwamba ipo haja ya kuchukua hatua zaidi. Jeshi la Polisi liliainisha sababu tatu kwenye barua ya katazo. Kwamba, Mhe. Rais hajadhibitisha kushiriki kwenye maandamano; kufanya maandamano umbali mrefu- Mwenge hadi Mnazi Mmoja kutaathiri shuguli kwa kufunga barabara na tarehe 30/Oktoba 2017 ni siku ambayo mitihani ya kidato cha nne itakuwa ikifanyika. Hivyo, taarifa ya kusudio la maandamano ikakataliwa.

Kwa sababu hizi zilizotumika kukataza maandamano, JUKATA tumefikia maamuzi ya kwenda kufungua kesi mahakamani kudai haki ambayo inaminywa na kukandamizwa na Jeshi la Polisi kwa kutumia sababu nyepesi. JUKATA ipo kwenye hatua za mwisho kutekeleza uamuzi huu na kwamba jopo la Mawakili wasomi wasiopungua kumi wakiongozwa na Dkt. Rugemeleza Nshala watahusika katika mchakato huu wa kudai mahakamani haki hii ya kufanya maandamano ya amani.

3. **KWA NINI NI MUHIMU KWENDA MAHAKAMINI**

Duniani kote katika nchi za kidemokrasia zinazofuata utawala wa sheria, Mhimili wa Mahakama ndicho chombo mahususi cha kutoa haki pale mtu ama watu wanapoona haki zao zimenyimwa ama zimekandamizwa. Hapa kwetu Tanzania, kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, toleo la mwaka 2005, **ibara ya 107 (A) (1**) inasema.. `***Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki***

JUKWAA LA KATIBA TANZANIA

katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama'. Kwa msingi huu wa kikatiba na kwa sababu Jeshi la Polisi limeendelea kuminya haki za kikatiba zinazopatikana kwenye katiba ya Tanzania ibara, 18 (a), (b), (d) pamoja na 20 (b), tunaona njia sahihi na ya kikatiba kudai haki hizi sisi kama sehemu ya watanzania ni kufikisha jambo hili mahakamani. Tunatarajia Mahakama itaeleza ni kwa namna gani wananchi wanapaswa kutumia haki zao za kikatiba bila kuzuiwa, kuwekewa vikwazo ama kusumbuliwa na Jeshi la Polisi.
Uzoefu kwingineko duniani, kama vile nchini Kenya, jirani yetu na mwanachama mwenzetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, pale inapotokea haki kama hizi zinaponyimwa ama kuzuiwa na Jeshi la Polisi ama mtu yeyote, imedhihirika kuwa wananchi wanapokwenda mahakamani kudai haki hizi, mahakama imekuwa ikifanya kazi yake vizuri kwa kuruhusu wananchi kutumia haki zao za kikatiba hasa kuandamana na kufanya mikutano ya hadhara. Tunataka nchi yetu pia iwe nchi yenye uvumilivu wa kidemokrasia na kuheshimu haki za binadam.

Aidha, sababu nyingine ya kwenda mahakamani ni kuomba tafsiri ya mahakama kuhusu namna Jeshi la Polisi linavyotumia vifungu 43 (3) na 44 vya Sheria ya Jeshi la Polisi ya Mwaka 2002. Kwa mtizamo na uchambuzi wetu, Jeshi la Polisi limekuwa likitumia vibaya vifungu hivi kuzuia mikutano pamoja na maandamano ya amani kinyume kabisa na uhalisia wa vifungu hivi kwa kisingizio cha uwepo wa taarifa za ***kiintelijensia*** kwamba kuna viashiria vya uvunjifu wa amani. Tunaamini, ni muda muafaka wa mahakama kuweza kusaidia kupatikana tafsiri sahihi ya vifungu hivi vinavyotumika vibaya kukandamiza haki.

UKWAZA KATIBA TANZANIA

4. MSIMAMO WA JUKATA

Kutokana na maoni yaliyokusanywa kutoka kwa wananchi na TWAWEZA pamoja na JUKATA juu ya mchakato wa katiba kuanzia mwezi Juni 2017 na taarifa kutolewa tarehe 19 Oktoba, JUKATA tunaendelea kusisitiza haja na umuhimu wa kukamilishwa kwa mchakato huu adhimu. Imethibitika wananchi asilimia 67% wanaona ni muhimu Tanzania kupata katiba mpya. Hivyo, ni muhimu sana serikali ikatekeleza jambo hili kwa kuwa pia lipo kwenye ilani ya uchaguzi ya chama tawala. Aidha, JUKATA tumesikitishwa sana na kauli yenye kupotosha kutoka kwa baadhi ya watu kwamba Tanzania kwa sasa inahitaji kujifunza ***Ukatiba*** na si kuandika katiba mpya. Hii kauli inapaswa kupingwa na wananchi wote kwa vile Ukatiba ni mwendelezo wa kuiishi katiba, hivyo tunahitaji katiba mpya ili wananchi waweze kuiishi hiyo katiba. Bila katiba mpya ya wananchi, ukatiba hauwezekani maana chimbuko la misingi ya kisiasa, kiutawala, kiuongozi, kijamii na kiuchumi inajengwa kwenye katiba.

Kwa upande mwingine, tunasisitiza serikali kufanya marekebisho kwenye katiba ya sasa endapo mchakato wa katiba mpya utakuwa haujakamilika mwaka 2020 wakati wa uchaguzi ili kuondoa dosari ambazo zimekuwa zikilamikiwa kila ufanyikapo uchaguzi. Tunaitaka serikali izingatie mapendekezo ya JUKATA kuhusu nini kifanyike endapo serikali itashindwa kukamilisha mchakato wa katiba mpya kabla ya uchaguzi mkuu wa 2020 tuliyoyatoa tarehe 16 Septemba 2017.

5. HITIMISHO

Nchi ya Tanzania inafuata misingi ya kidemokrasia na utawala wa sheria. Misingi mikuu ya demokrasia ni pamoja na uhuru wa watu kukusanyika na kujadiliana kwa mujibu wa sheria masuala yanayohusu taifa lao. Misingi ya demokrasia inapominywa ama

JUKWAA LA KATIBA TANZANIA

kukandamizwa na vyombo vya dola, watu ama vikundi waathirika wakubwa ni wananchi ambao ndio msingi wa mamlaka yote. Na kwa vile serikali inapata mamlaka kutoka kwa wananchi, lengo la serikali sharti liwe ni ustawi wa wananchi ambapo serikali itawajibika kwa wananchi. Kwa sasa, zipo kauli nyingi kutoka kwa wananchi juu ya kufifia kwa demokrasia na ukiukwaji wa haki za binadam. JUKATA tunaendelea kusisitiza umuhimu wa serikali, vyombo vya dola na wananchi kwa ujumla kuheshimu sheria na taratibu zilizowekwa ili kuongoza nchi, haya yote yatajengeka kwenye katiba iliyo bora itokanayo na wananchi wenyewe.

Imetolewa na JUKATA na kusainiwa na;

Hebron Mwakagenda

Mwenyekiti

04/11/2017

JUKWAA LA KATIBA TANZANIA